

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA
DARASA LA NNE (SFNA) 2018**

01 KISWAHILI

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA
DARASA LA NNE (SFNA) 2018**

01 KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

| | |
|---|----|
| DIBAJI | iv |
| 1.0 UTANGULIZI | 1 |
| 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI..... | 3 |
| 2.1 Sehemu A:..... | 3 |
| 2.2 Sehemu B:..... | 7 |
| 2.3 Sehemu C: | 12 |
| 2.4 Sehemu D: | 16 |
| 2.5 Sehemu E:..... | 19 |
| 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA UMAHIRI MBALIMBALI | 26 |
| 4.0 HITIMISHO | 27 |
| 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO | 27 |
| KIAMBATISHO CHA PEKEE | 29 |

DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Upimaji wa Darasa la Nne 2018 imezingatia muhtasari mpya wa mtaala wa somo la Kiswahili ulioandaliwa mwaka 2016 kwa darasa la tatu hadi la nne (III-IV). Maswali ya Upimaji yaliandaliwa kwa kutumia mwongozo mpya wa mwaka 2018 uliozingatia mabadiliko ya muhtasari wa somo la Kiswahili. Umahiri wa wanafunzi umepimwa kwa kuzingatia viwango mbalimbali vya kufaulu ambao umegawanyika katika kiwango hafifu, kiwango cha wastani, kiwango kizuri na kiwango kizuri sana.

Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wadhibiti ubora wa elimu, waandaaji wa mitaala na wadau wengine wa elimu. Aidha, taarifa hii inaonesha jinsi mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji uliyoyomwezesha au kushindwa kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka minne ya elimu ya msingi.

Sambamba na hayo, taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa usahihi Baadhi ya sababu hizo ni kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa maarifa na athari ya lugha mama. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi huu kwa kutumia maelezo, vielelezo na chati.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa taarifa hii itawawezesha wanafunzi na wasimamizi wa elimu kubuni mbinu zitakazosaidia kuimarisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi yatasaidia kuongeza umahiri wa wanafunzi na hatimaye kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa nchini.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii wakiwemo maafisa mitihani, wataalamu wa TEHAMA na wataalamu wengine wa elimu. Baraza linatarajia kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu ili kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Upimaji wa Kitaifa kwa wanafunzi wa Darasa la Nne.



Dkt. Charles E. Msonde

KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho wa namna ambavyo wanafunzi walijibu maswali ya upimaji wa somo la Kiswahili mwezi Novemba 2018. Upimaji huu ni wa kwanza katika mtaala mpya wa darasa la III- IV wa mwaka 2016 unaozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi katika stadi ya *kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika*.

Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na sehemu tano ambazo ni A: *Umahiri wa mwanafunzi katika kusikiliza matamshi ya silabi, maneno na sentensi na kuyaandika (Imla)*. B: *Umahiri wa mwanafunzi wakutumia maumbo ya umoja na wingi wa maneno na sentensi katika mawasiliano*. C: *Umahiri wa mwanafunzi kutumia lugha ya methali na nahau katika mawasiliano mbalimbali*. D: *Umahiri wa mwanafunzi kutumia alama za uandishi katika mawasiliano na* E: *Umahiri wa mwanafunzi katika kusoma na kubaini kwa usahihi hoja kuu*. Sehemu hizo tano zimetoka katika umahiri mkuu ambao ni *kuwasiliana katika miktaadha mbalimbali na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*.

Kila sehemu ilikuwa na swali **moja (1)** lenye vipengele **vitano (5)** vyenye jumla ya alama **kumi (10)**. Jumla ya wanafunzi **1,362,523** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na waliopimwa katika somo la Kiswahili walikuwa **1,300,456**. Aidha, wanafunzi **1,148,624** sawa na asilimia **88.33** ndiyo waliofaulu katika upimaji huo.

Viwango vya kufaulu kwa wanafunzi vimegawanyika katika makundi manne kulingana na alama walizopata ambapo kiwango hafifu ni 0 -2,

wastani 4 – 6, mzuri 8 na kiwango kizuri sana cha kufaulu ni alama 10. Wanafunzi waliopata kiwango cha wastani, kizuri na kizuri sana walihesabika kuwa wameweza kujibu swali. Aidha waliopata kiwango hafifu cha kufaulu walihesabika kuwa wameshindwa kujibu swali. Hata hivyo, kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika taarifa hii kimeainishwa kuwa ni hafifu, wastani au kizuri iwapo asilimia ya wanafunzi waliofaulu upimaji wako kati ya kundi la 0 – 33, 34 – 66 na 67 – 100. Vile vile taarifa hii imeainisha sababu za kufaulu au kutofaulu kwa wanafunzi kwa kila swali. Sampuli za majibu hafifu na mazuri zimetumika kuonesha viwango vya kufaulu kwa baadhi ya wanafunzi katika baadhi ya maswali. Aidha chati zimetumika kuonesha kufaulu kwa wanafunzi katika kila swali.


2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Sehemu hii inachambua maswali yaliyoulizwa na majibu waliyoandika wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwa kila sehemu. Aidha, idadi na asilimia ya wanafunzi walioweza au kushindwa kuandika jibu sahihi imewasilishwa katika chati na vielelezo. Vilevile sababu zilizochangia wanafunzi kujibu au kushindwa kujibu maswali zimefafanuliwa. Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi kimetafsiriwa kuwa ni “kizuri” ikiwa theluthi mbili ya wanafunzi waliopimwa wameandika jibu sahihi. Kwa upande mwengine, kiwango “hafifu” ni pale ambapo theluthi mbili ya wanafunzi waliofanya upimaji wameshindwa kuandika jibu sahihi. Hali kadhalika, iwapo theluthi au chini ya theluthi mbili ya wanafunzi waliopimwa wamepata jibu sahihi, basi kiwango cha kufaulu kitakuwa cha wastani.

2.1 Sehemu A:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la imla na mwanafunzi alitakiwa kusikiliza kwa makini sentensi alizosomewa kisha kuziandika kwa usahihi. Mwanafunzi alipaswa kusikiliza na kuandika sentensi tano zenye jumla ya alama 10. Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi kusikiliza na kuandika sentensi kwa usahihi. Jumla ya wanafunzi 1,300,456 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 1,180,364 sawa na asilimia 90.3 walifaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 10. Viwango vya kufaulu katika swali hili vimeainishwa katika

Chati Na. 2.1.1



Chati Na. 2.1 1 Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia.

Swali la 1:Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

- (i) _____
- (ii) _____
- (iii) _____
- (iv) _____
- (v) _____

Zifuatazo ni sentensi walizosomewa wanafunzi:

- (i) Baba ni fundi seremala.
- (ii) Kila asubuhi ninakunywa uji.
- (iii) Mwalimu wetu ni mshereheshaji.
- (iv) Bustani yetu imepandwa maua.
- (v) Mgeni ameporwa mali zake.

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 720,594 sawa na asilimia 55.4 walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwa kupata alama zote 10. Wanafunzi hao waliweza kubaini sauti za maneno yote yaliyosomwa na kuyaandika kwa usahihi huku wakizingatia alama za uandishi pamoja na kutumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi. Aidha, waliweza kuandika kwa usahihi sauti /r/ na /l/ zilizokuwa zinaunda baadhi ya maneno katika sentensi, kwa mfano, neno “seremala” katika kipengele cha kwanza (i). Pia, waliweza kuelewa na kuandika silabi zenye herufi mwambatano, kwa mfano “-nywa” katika kipengele (ii). Kwa jumla, wanafunzi hawa walikuwa na umahiri wa kusikiliza na kuandika sauti za herufi za maneno pamoja na alama za uandishi kwa usahihi. **Kielelezo 2.1.1** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (5) vy a swali hili.

Kielelezo Na. 2.1.1

1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.**
 - (i) Baba ni fundi Sremala.
 - (ii) Kila asubuhi pinakunywa uji.
 - (iii) Mwalimu wetu ni Msherehehaji.
 - (iv) Bustani yetu imepandua maua
 - (v) Mgeni amepirula mali zake.

Kielelezo 2.1.1: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeeweza kujibu vipengele vyote vy a swali kwa usahihi.

Aidha, wanafunzi 391,489 sawa na asilimia 30.1 walifaulu kwa kiwango kizuri ambapo waliweza kuandika kwa usahihi maneno 13 hadi 19 kwa sentensi zote tano na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi

hao walikuwa na umahiri wa kusikiliza pamoja na kuandika matamshi ya silabi za sentensi walizosomewa. Pia, walizingatia matumizi ya alama za uandishi ingawa wengine walionekana kushindwa kutambua silabi zenyenye herufi mwambatano. Kwa mfano wapo walioshindwa kuandika “*ninakunywa*” na kuandika kimakosa “*nina*” “*kunywa*”.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 68,281 sawa na asilimia 4.8 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwani waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 12 kwa sentensi zote tano na kupata alama kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya matumizi ya alama za uandishi ingawa walishindwa kuandika baadhi ya maneno yenye silabi mwambatano pamoja na kuchanganya herufi / na r. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika “*selemala*” badala ya “*seremala*”.

Hali kadhalika, wanafunzi 120,113 sawa na asilimia 9.2 walipata kiwango hafifu cha kufaulu. Miogoni mwao wapo walioshindwa kabisa kuandika hata neno moja na walioweza kuandika kwa usahihi neno moja na kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5 kwani hawakuwa na stadi ya kusoma na kuandika. Wanafunzi hao walishindwa kusikiliza na kuandika sauti za herufi za maneno ambazo zinaunda silabi ili kukamilisha neno na sentensi. **Kielelezo 2.1.2** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi alireshindwa kuandika maneno aliyo somewa kwa kukosa stadi ya kusoma na kuandika.

Kielelezo Na. 2.1.2

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) BABA, nizuse mura

(ii) kiaasubu

(iii) sHele muSana


(iv) Busitini s

(v) matKilini

Kielelezo 2.1.2: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuandika maneno aliyosomewa kwa kukosa stadi ya kusoma na kuandika.

2.2 Sehemu B:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano ambavyo vililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kuhusu dhana ya umoja na wingi. Kila kipengele kilikuwa na alama 2 ambapo swali lilikuwa na jumla ya alama 10. Swali limetoka katika umahiri mkuu wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima ujuzi wa mwanafunzi wa kubaini matumizi ya vipashio vya umoja na wingi katika sentensi. Jumla ya wanafunzi 1,300,456 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 1,051,453 sawa na asilimia 80.8 waliweza kujibu kwa usahihi maneno 6 hadi 20 na kupata alama kuanzia 3 hadi 10. Viwango vya kufaulu katika swali hili vimeainishwa katika **Chati Na. 2.2.1**



Chati Na. 2.2.1: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia.*

Swali la 2: Andika umoja na wingi wa sentensi zifuatazo; kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.

- (i) Umoja: Kiti chake kimevunjika.
Wingi: Viti vyake vimevunjika.
- (ii) Umoja: Hiki ni kitabu changu.
Wingi: _____
- (iii) Umoja: Kiatu changu cheupe kimepotea.
Wingi: _____
- (iv) Umoja: _____
Wingi: Wapishi wamepika chakula kitamu.
- (v) Umoja: Kalamu yako ilipotea darasani.
Wingi: _____
- (vi) Umoja: _____
Wingi: Miti hii ilianguka juzi.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 197,114 sawa na asilimia 15.2 walikuwa na kiwango kizuri sana cha

kufaulu. Wanafunzi hao waliweza kuandika kwa usahihi maneno yote 20 na kupata alama zote 10. Waliweza kubaini maumbo ya umoja na wingi katika majina ya Kiswahili kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kwa mfano, katika kipengele (i) *Hiki ni kitabu changu* jibu lake katika wingi ni *Hivi ni vitabu vyangu* na kipengele (ii) *Kiatu changu kimepotea* ambapo wingi wake ni *Viatu vyangu vimepotea*. Sentensi hizi mbili zimetoka katika maumbo ya *KI – VI* yanayoonesha umoja na wingi katika sentensi. Hivyo, wanafunzi walikuwa na umahiri wa kutambua vipashio vinavyokamilisha maumbo ya umoja na wingi katika sentensi. **Kielelezo 2.2.1** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeeweza kubaini maumbo ya umoja na wingi katika sentensi.

Kielelezo Na. 2.2.1

- | | |
|--|--|
| 2. Andika umoja au wingi wa sentensi zifuatazo; kipengele cha (i) kimetumika kama mfano. | |
| (i) Umoja | Kiti chake kimevunjika. |
| Wingi | <u>Viti vyake vimevunjika.</u> |
| (ii) Umoja: | Hiki ni kitabu changu. |
| Wingi: | <u>Hivi ni vitabu vyetu</u> |
| (iii) Umoja: | Kiatu changu cheupe kimepotea. |
| Wingi: | <u>Viatu vyangu vyeupe vimepotea.</u> |
| (iv) Umoja: | <u>Mpishi amepika chakula kitamu.</u> |
| Wingi: | Wapishi wamepika chakula kitamu. |
| (v) Umoja: | Kalamu yako ilipotea darasani. |
| Wingi: | <u>Kalamu zako zimepotea darasani.</u> |
| (vi) Umoja: | <u>Miti huu ulianguka juzi</u> |
| Wingi: | Miti hii ilianguka juzi. |

Kielelezo 2.2.1: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeeweza kubaini maumbo ya umoja na wingi katika sentensi.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 651,303 sawa na asilimia 50.0 walifaulu kwa kiwango kizuri ambapo waliweza kuandika kwa usahihi maneno 13 hadi 19 na kupata kuanzia alama 6.5 hadi 9.5. Waliweza kubaini maumbo ya umoja na wingi katika sentensi. Kwa mfano waliweza kuandika sentensi katika wingi; Mti huu ylianguka wingi wake ni miti hii jlianguka. Hata hivyo, wapo wanafunzi walioshindwa kubaini kuwa umoja na wingi wa sentensi unatokana na maumbo ya *U-* ambapo kipashio *-u-* kipo katika umoja na *-i-* ni cha wingi hivyo kushindwa kuandika maumbo ya umoja na wingi katika baadhi ya sentensi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 203,036 sawa na asilimia 15.6 walifaulu kwa kiwango cha wastani. Hawa waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 12 kwa sentensi zote tano na kupata alama kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kubaini maumbo ya umoja na wingi katika sentensi ingawa walikuwa na changamoto ya kuchanganya vipashio vya maumbo hayo. Baadhi ya wanafunzi walichanganya dhana ya umoja na wingi kwa baadhi ya maneno katika sentensi. Walishindwa kubaini kuwa umbo ki katika umoja linakuwa yi ili kupata umbo la wingi wa sentensi. Kwa mfano, umoja; Kiatu changu cheupe kimepotea, wingi Kiatu vyangu cheupe kimepotea.

Aidha, wanafunzi 24,913 sawa na asilimia 19.2 walipata alama 0 hadi 2.5 kwa kuwa walishindwa kubaini matumizi ya vipashio vya umoja na wingi katika sentensi. Vilevile, walishindwa kuandika sentensi hizo kwa usahihi kutokana na athari ya lugha mama. Kwa mfano, katika kipengele (ii) *Hiki ni kitabu changu*, mwanafunzi mmoja aliandika *ivi ni vitabu vwangu*. Majibu hayo yanaonesha kuwa, mwanafunzi huyo ameathiriwa na lugha mama. **Kielelezo 2.2.2** kinaonesha sampuli ya

majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kubaini vipashio vya umoja na wingi pamoja na athari ya lugha mama.

Kielelezo Na. 2.2.2

2. Andika umoja au wingi wa sentensi zifuatazo; kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.

(i) Umoja Kiti chake kimevunjika.

Wingi Viti vyake vimevunjika.

(ii) Umoja: Hiki ni kitabu changu.

Wingi: vini nii vitabu vwangu.

(iii) Umoja: Kiatu changu cheupe kimepotea.

Wingi: vitabu vwangu vime potea.

(iv) Umoja: na wingi

Wingi: Wapishi wamepika chakula kitamu.

(v) Umoja: Kalamu yako ilipotea darasani.

Wingi: Kalamu yako imepotea darasani.


(vi) Umoja: miti hii ime nyaulgu.

Wingi: Miti hii ilianguka juzi.

Kielelezo 2.2.2: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kubaini vipashio vya umoja na wingi pamoja na kuathiriwa na lugha mama.

2.3 Sehemu C:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitatu (3) na lililenga kupima umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali. Mwanafunzi alipimwa umahiri wa kutumia methali na nahau ili kuwasiliana katika miktadha mbalimbali. Jumla ya wanafunzi 1,300,456 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili lenye jumla ya alama 10. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo wanafunzi 514,992 sawa na asilimia 39.6 waliweza kujibu vipengele 2 hadi 5 na kupata kuanzia alama 4 hadi 10. Viwango vyta kufaulu katika swali hili vimeainishwa katika **Chati Na. 2.3.1**



Chati Na: 2.3.1 Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia

Swali la 3:

- (a) Kamilisha methali ulizopewa kwa **kuandika jibu sahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Fahali wawili_____

(ii) Mvumilivu,_____

(b) Toa maana ya methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:

(i) Kidole kimoja hakivunji chawa _____

(ii) Ahadi ni deni _____

(c) Nahau "tia doa" ina maana gani? _____

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 785,511 sawa na asilimia 60.4 walipata alama 0 na 2 kwani walikosa maarifa kuhusu dhana ya methali na nahau za Kiswahili. Kwa mfano, katika kipengele (a) mwanafunzi alitakiwa akamilishe methali (i) *fahali wawili*____na (ii) *mvumilivu*_____. Mwanafunzi mmoja alijibu "*wanyama*" katika kipengele (i) kwa kuhawilisha maarifa kuwa fahali ni madume ya ng'ombe. Katika kipengele (ii) alijibu "*umoja*" kwa kuwa hakuwa na maarifa ya kukamilisha methali. Hata hivyo, wapo wanafunzi walioweza kujibu kipengele kimoja cha swali na kupata alama 2. **Kielelezo 2.3.1** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukamilisha muundo wa methali pamoja na kueleza maana ya methali na nahau.

Kelelezo Na.2.3.1

| | |
|----|--|
| 3. | (a) Kamilisha methali ulizopewa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi: (i) Fahali wawili, <u>wanyama</u> (ii) Mvumilivu, <u>Umuja</u> |
| | (b) Toa maana ya methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi: (i) Kidole kimoja hakivunji chawa <u>Kinanunjika</u> (ii) Ahadi ni deni <u>Hakudai fena</u> |
| | (c) Nahau "tia doa" ina maana gani? <u>Hudon dasha</u> |

Kielelezo 2.3.1: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukamilisha muundo wa methali pamoja na kutoa maana ya methali na nahau.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 432,837 sawa na asilimia 33.3 walipata kiwango cha wastani cha kufaulu. Waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 2 au 3 kwa sentensi zote tano na kupata alama 4 au 6. Vilevile, walishindwa kukamilisha maana ya baadhi ya methali na nahau kwa kukosa maarifa pamoja na kutoelewa dhana ya lugha ya picha.

Hali kadhalika, wanafunzi 63,070 sawa na asilimia 4.8 walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu ambapo waliweza kujibu vipengele 4 kati ya vitano na kupata alama 8. Aidha, baadhi yao walishindwa kueleza

muundo na maana ya methali pamoja na nahau. Kwa mfano waliandika kimakosa maana ya *tia doa ni kudondosha*.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 19,085 sawa na asilimia 1.5 walipata kiwango kizuri sana cha kufaulu. Wanafunzi hao waliweza kukamilisha methali pamoja na kutoa maana ya methali na nahau kwa usahihi. Mfano katika kipengele (a) mwanafunzi alijibu (i) *Fahali wawili hawaishi zizi moja*, (ii) *Mvumilivu hula mbivu*. Katika kipengele (b) (i) *Kidole kimoja hakivunji chawa jambo bila ushirikiano halifanyiki*. **Kielelezo 2.3.2** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele 5 vya swali kwa usahihi.


Kielelezo Na 2.3.2

3. (a) Kamilisha methali ulizopewa kwa **kuandika jibu sahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi:
- (i) Fahali wawili, Hawaishi zizi moja
(ii) Mvumilivu, hula mbivu
- (b) Toa maana ya methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:
- (i) Kidole kimoja hakivunji chawa
Jambo bila ushirikiano halifanyiki
- (ii) Ahadi ni deni Mtu ukimwambia utamfanyia
kitu ni lazima ukifanya
- (c) Nahau "tia doa" ina maana gani?
maana yake kuharibu

Kielelezo 2.3.2: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kukamilisha methali na nahau pamoja na kueleza maana zake.

2.4 Sehemu D:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kipengele kina alama 2 na kufanya jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na lililenga kupima umahiri wa wanafunzi katika kutumia alama za uandishi. Swali lilijibowi na wanafunzi 1,300,389 sawa na asilimia 100. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo jumla ya wanafunzi 547,867 sawa na asilimia 42.1 waliweza kujibu vipengele viwili hadi 5 na kupata alama kuanzia 4 hadi 10. Viwango vya kufaulu katika swali hili vimewasilishwa katika **Chati Na. 2.4.1**



Chati Na. 2.4.1: Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia.

Swali la 4: Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi ilioachwa wazi.

- (i) Je _____ utafika saa ngapi _____
- (ii) Embe _____ nanasi na papai ni matunda _____

- (iii) Loo _____ kwani wewe ni nani _____
- (iv) Oyee _____ nani amefunga goli _____
- (v) Haba na haba _____ hujaza kibaba _____

Wanafunzi 752,522 sawa na asilimia 57.9 waliweza kujibu kipengele 1 au kushindwa kabisa na kupata alama kuanzia 0 hadi 2. Baadhi yao hawakuwa na umahiri wa kubaini alama stahiki za uandishi ambapo waliandika maneno badala ya alama. Mfano katika kipengele (i) Je rudi utafika saa ngapi saa hivi. **Kielelezo 2.4.1** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika maneno badala ya alama za uandishi.

Kielelezo Na. 2.4.1

4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:
- (i) Je rudi utafika saa ngapi Sasa hivi
 - (ii) Embet likiti nanasi na papai ni matunda matamu
 - (iii) Loo huyu kwani wewe ni nani Mtu
 - (iv) Oyee Vipa nani amefunga goli ronaldo
 - (v) Haba na haba Samu hujaza kibaba Kitendawili

Kielelezo 2.4.1: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeandika maneno badala ya alama za uandishi.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 308,431 sawa na asilimia 23.7 walifaulu kwa kiwango cha wastani. Waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 2 vya swali na kupata alama kuanzia 4 hadi 6.

Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kubaini alama za uandishi japo walichanganya dhana ya alama za uandishi na maneno. **Kielelezo 2.4.2** kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyechanganya alama za uandishi na herufi za maneno.

Kielelezo Na. 2.4.2

4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyooachwa wazi:
- (i) Jc a utafika saa ngapi p
 - (ii) Embe s nanasi na papai ni matunda ?
 - (iii) Loo H kwani wewe ni nani i
 - (iv) Oyee l nani amefunga goli ?
 - (v) Haba na haba ll hujaza kibaba •

Kielelezo 2.4.2: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyechanganya herufi na alama za uandishi.

Vilevile, wanafunzi 170,917 sawa na asilimia 13.1 walipata kiwango kizuri cha kufaulu. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 4 na kupata alama 8. Baadhi yao walishindwa kubaini na kutumia alama stahiki za uandishi na kuandika maneno badala ya alama za uandishi. Kwa mfano mwanafunzi mmoja aliandika “*kipa*” badala ya kuweka alama ya (!).

Uchambuzi wa kina unaonesha kuwa, wanafunzi 68,519 sawa na asilimia 5.3 walifaulu kwa kiwango kizuri sana. Waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano kwa kuweka alama stahiki za uandishi katika sentensi na kupata alama zote 10. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutumia lugha katika kuwasiliana kwa kuzingatia kanuni za lugha ya maandishi. Hii ina maana kuwa, wanaelewa matumizi ya alama za uandishi zilizopimwa. **Kielelezo 2.4.3** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeeweza kutumia alama za uandishi.

Kielelezo Na. 2.4.3

4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi:
- (i) Je 9 utafika saa ngapi ?
 - (ii) Embe 9 nanasi na papai ni matunda .
 - (iii) Loo ! kwani wewe ni nani ?
 - (iv) Oyee ! nani amefunga goli ?
 - (v) Haba na haba , hujaza kibaba .


Kielelezo 2.4.3: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeeweza kuandika alama za uandishi katika sentensi.

2.5 Sehemu E:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama 10. Swali lililenga kupima umahiri wa kuonesha uelewa wa jambo ambalo mwanafunzi amelisikia au kulisoma. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi wa kusoma na kubaini hoja kuu katika shairi. Jumla ya wanafunzi 1,300,456 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kiwango cha kufaulu katika swali hili ni kizuri ambapo wanafunzi 998,417 sawa na asilimia 76.8 waliweza kupata alama kuanzia 4 hadi

10. Viwango vya kufaulu katika swali hili vimeainishwa katika **Chati Na.**

2.5.1



Chati Na. 2.5.1: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia.*

Swali la 5: Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Nchi yangu naipenda, hakika nawaeleza,
Ni nchi yenye matunda, huwezi kuyamaliza,
Na asali tunapenda, nchi yajitokeza,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Kuna mrefu mlima, Kilimanjaro twakwea,
Ardhi ya wakulima, rutuba imeenea,
Pia mbuga za wanyama, Mikumi nawaambia,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Tamati ninaishia, mengi nimewaeleza,
Kabla sijaishia, mito ninawaeleza,
Bahari pia sikia, na maziwa yapendeza,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Maswali

- (a) Nini maana ya neno “tamatii” kama lilivyotumika katika ubeti wa tatu?

-
- (b) Shairi hili linahusu nini?

-
- (c) Taja mlima mrefu uliotajwa na mshairi.

-
- (d) Taja mbuga ya wanyama iliyotajwa katika shairi.

-
- (e) Taja vyanzo viwili vya maji vilivyotajwa katika shairi hili.

(i) _____

(ii) _____

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 480,352 sawa na asilimia 37.0 walifaulu kwa kiwango cha wastani. Wanafunzi hao waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 vya sentensi tano na kupata alama 4 au 6. Aidha, walishindwa kujibu vipengele vingine kwa kukosa umahiri wa kusoma na kubaini yaliyomo katika shairi. Kwa mfano, walipoulizwa wataje mlima mrefu uliotajwa katika shairi, baadhi yao walijibu kuwa, ni “*serengeti*”, wengine “*twakwea*”, “*mlima mrefu*” na wengine “*mito na bahari*.”

Vilevile, wanafunzi 348,555 sawa na asilimia 26.8 walifaulu kwa kiwango kizuri kwani waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 4 kati ya 5 na kupata alama 8. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kusoma na kupambanua yaliyomo ndani ya shairi ingawa baadhi yao walikosa weledi wa kubaini wazo kuu. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi

walishindwa kutaja mlima mrefu, vyanzo viwili vya maji, mbuga ya wanyama na maana ya neno tamati.

Hali kadhalika, wanafunzi 302,057 sawa na asilimia 23.2 walipata kiwango hafifu cha kufaulu. Wanafunzi hao walipata alama 0 au 2 kwani hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuwasilisha mawazo yaliyotolewa katika shairi. Baadhi yao walinakili baadhi ya mistari ya shairi katika kipengele (a) hadi (e). **Kielelezo 2.5.2** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyenakili mistari ya shairi badala ya kujibu maswali.

Kielelezo 2.5.1

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Nchi yangu naipenda, hakika nawaeleza,
Ni nchi yenye matunda, huwezi kuyamaliza,
Na asali tunapenda, nchini yajitokeza,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Kuna mrefu mlima, Kilimanjaro twakwca,
Ardhi ya wakulima, rutuba imeneea,
Pia mbuga za wanyama, Mikumi nawaambia,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Tamati ninaishia, mengi nimewacleza,
Kabla sijaishia, mito ninawaeleza,
Bahari pia sikia, na maziwa yapendeza,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Maswali

- (a) Nini maana ya neno "tamati" kama lilivyotumika katika ubeti wa tatu?

Tamati ninaishia mengi ni newaeleza

- (b) Shairi hili linahusu nini?

Ninchi yenye matunda huwezi kuyamaliza

- (c) Taja mlima mrefu uliotajwa na mshairi.

No asali tunapenda nchini yajitokeza
(d) Taja mbuga ya wanyama iliyotajwa katika shairi
hili. Kabla sijaishia mito

- (e) Taja vyanzo viwili vya maji vilivyotajwa katika shairi hili.

(i) Tanzania Tanzania nchi yangu na kupenda
(ii) Bahari pia sikia na maziwa yapendeza

Kielelezo 2.5.1: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyenakili mistari ya shairi badala ya kujibu maswali.

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 169,510 sawa na asilimia 13 walifaulu kwa kiwango kizuri sana. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano kwenye shairi na kupata alama 10. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusoma shairi kwa ufahamu na kubaini yaliyomo ndani yake. Aidha, walionesha umahiri katika stadi ya kuandika kwa kuwa waliweza kuandika majibu ya maswali waliyoulizwa kwa usahihi. Kwa mfano, katika kipengele (a) kilichomtaka mwanafunzi aelete maana ya neno “*tamati*” kama ilivyotumika katika ubeti wa tatu, mwanafunzi mmoja alijibu kwa usahihi kuwa ni *mwisho*. Kwa jumla, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na umahiri wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika shairi. **Kielelezo 2.5.2** sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyweweza kubainisha majibu kutokana na shairi alilolisoma.

Kielelezo Na. 2.5.2

5. Soma kwa makini shairi lifuatato kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Nchi yangu naipenda, hakika nawaeleza,
Ni nchi yenye matunda, huwezi kuyamaliza,
Na asali tunapenda, nchini yajitokeza,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Kuna mrefu mlima, Kilimanjaro twakwea,
Ardhi ya wakulima, rutuba imeenea,
Pia mbuga za wanyama, Mikumi nawaambia,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Tamati ninaishia, mengi nimewaeleza,
Kabla sijaishia, mito ninawaeleza,
Bahari pia sikia, na maziwa yapendeza,
Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Maswali

- (a) Nini maana ya neno "tamati" kama lilivyotumika katika ubeti wa tatu?

Maana ya neno "tamati" ni mwisho.

- (b) Shairi hili linahusu nini?

Shairi hili linahusu nchi ya Tanzania.

- (c) Taja mlima mrefu uliotajwa na mshairi.

Mlima mrefu uliotajwa na mshairi ni mlima Kilimanjaro.

- (d) Taja mbuga ya wanyama iliyotajwa katika shairi

hili. Mikumi ni mbuga ya wanyama iliyotajwa katika shairi hili.

- (e) Taja vyanzo viwili vya maji vilivyotajwa katika shairi hili.

(i) Bahari

(ii) Mkuu

Kielelezo 2.5.2: kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kusoma na kujibu maswali yaliyotokana na shairi kwa usahihi.

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA UMAHIRI MBALIMBALI

Upimaji wa somo la Kiswahili umehusisha umahiri katika stadi za lugha ambazo zimejitokeza katika vipengele vitano (5). Vipengele hivyo ni kusikiliza matamshi ya silabi, maneno na sentensi kisha kuyaandika (Imla), kutumia maumbo ya umoja na wingi wa sentensi katika mawasiliano, kutumia lugha ya methali na nahau, kutumia alama za uandishi katika mawasiliano mbalimbali pamoja na kusoma kwa ufahamu ili kubaini hoja kuu.

Uchambuzi zaidi wa viwango vya kufaulu kwa maswali unaonesha kuwa kuna maswali ambayo yalijibowi vizuri sana, vizuri, wastani na kwa uhafifu. Mathalan, swali la 1, ambalo lilipima umahiri wa mwanafunzi kusikiliza matamshi ya silabi, maneno na sentensi lilijibowi vizuri kwa asilimia 90.3. Aidha, swali la 2 lililopima umahiri wa mwanafunzi kutumia maneno/sentensi za umoja na wingi katika kuwasiliana lilijibowi vizuri kwa asilimia 80.8. Vilevile, swali la 3, lililopima umahiri wa mwanafunzi kutumia lugha ya picha (methali na nahau) katika kuwasiliana lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha kufaulu asilimia 39.6. Swali la 4, lilipima uwezo wa mwanafunzi kutumia alama za uandishi ambapo kiwango cha kufaulu kilikuwa cha wastani kwa asilimia 42.1. Swali la 5 lililopima umahiri wa mwanafunzi wa kusoma na kubaini ujumbe uliopo katika shairi lilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa asilimia 76.8.

Kwa sababu hiyo, swali la 1 lilikuwa na kiwango kizuri zaidi cha kufaulu kwa asilimia 90.3, wakati swali la 3 lilikuwa na kiwango cha chini cha kufaulu kati ya maswali yote kwa asilimia 39.6. Kwa ujumla, wanafunzi walifaulu zaidi kwa asilimia 76.8 katika umahiri wa kuonesha uelewa

wa jambo alilolisikiliza au kulisoma. Uchambuzi wa viwango vyatufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri umewasilishwa katika **kiambatisho cha pekee**.

4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa kwa jumla kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri. Hata hivyo, pamoja na kiwango cha kufaulu kuwa kizuri, zipo changamoto mbalimbali zilizosababisha wanafunzi wasiweze kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Baadhi ya changamoto hizo ni kushindwa kuelewa matakwa ya swali, athari ya lugha mama pamoja na kushindwa kumudu stadi za kusoma na kuandika.

Ingawa kumekuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, bado juhudu zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ili kuwajengea wanafunzi umahiri madhubuti utakaowawezesha kukabiliana na kasi ya ongezeko la matumizi ya lugha hii adhimu katika nyanja mbalimbali kitaifa na kimataifa.

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha inayoenye kwa kasi duniani, ni vyema lugha hii uwekewe misingi imara itakayowezesha ujifunzaji wake kuwa bora. Misingi hiyo inapaswa kuimarishwa kuanzia shule za awali hadi vuyo vikuu. Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne, mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

- (a) Walimu wertilie mkazo ufundishaji wa mbinu za kusikiliza na kuandika imla.
- (b) Walimu wabuni mbinu bora za kufundisha wanafunzi kusoma na kuandika.
- (c) Walimu wawajengee wanafunzi misingi imara kuhusu matumizi ya maumbo ya umoja na wingi wa sentensi katika kuwasiliana.
- (d) Walimu wawaelekeze wanafunzi mbinu za kutumia lugha ya picha katika kuwasiliana.
- (e) Walimu wawahimize wanafunzi kushiriki katika mashindano mbalimbali ya uandishi wa insha za Kiswahili ili kuwajengea umahiri wa kusoma habari na kubaini ujumbe uliomo.

KIAMBATISHO CHA PEKEE

MUHTASARI WA UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA SOMO LA KISWAHILI KWA KILA UMAHIRI

| Na | Umahiri Mkuu | UPIMAJI WA 2018 | | | |
|----|--|------------------------|-----------------|--------------------------|---------|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya kufaulu | | |
| 1 | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 5 | 76.8 | 76.8 | Mzuri |
| 2 | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 90.3 | 63.2 | Wastani |
| | | 2 | 80.8 | | |
| | | 3 | 39.6 | | |
| | | 4 | 42.1 | | |
| | | | | | |

